

NIBEBE

[sauti ya mtoto akilia kwa nguvu]

MAMA: Khe sara mbona mwanao Analia.

SARA: Mama, Hataki nimbebe, nafua ananisumbua.

MAMA: Muache acheze wakati unaendelea kufua.

SARA: Ni msumbufu tu, eti na yeye anataka afue.

MAMA: Vizuri, ni kwasababu ana akili na anataka kujifunza. Watoto wanajifunza kwa kuiga vitu unavyofanya.

SARA: Kwahio kucheza na mtoto wa miezi nane ni kitu kizuri?

MAMA: Ndio, na unaweza kucheza nae hata ukiwa unafanya kazi zingine. Kwanini usimpe kopo la maji achezee ukiwa unafua itamsaidia.

SARA: Kweli?

MAMA: Ndio. haya mjukuu wangu chukua hili kopo uchezee, wewe unataka kufua?

[Sauti ya kopo likigongwa + Sauti ya mtoto akifurahi]

MAMA: Si unaona alivyo furahi na kujiamini.

SARA: Ndio siri ya kuwa na mtoto mwenye akili eh?

MAMA: Ni moja ya siri, pia unatakiwa uongee, kuimba na kucheza nae ili uijenge akili yake.

SARA: Sasa nimeelewa. Mwanangu atakua na akili kama bibi yake.

Wazazi na walezi, anza kuongea, kucheza, kuimba na kumwonyesha upendo mtoto tangu anapozaliwa. Unamsaidia kukua kiakili na atakuwa mtoto mwerevu.